**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KILIMO**

**MAMLAKA YA AFYA YA MIMEA NA VIUATILIFU TANZANIA**

TANZANIA PLANT HEALTH AND PESTICIDES AUTHORITY

# TAARIFA KWA UMMA

## KUANZA KUTUMIKA KWA MFUMO WA FORODHA WA TANCIS KWA MAMLAKA YA AFYA YA MIMEA NA VIUATILIFU IFIKAPO TAREHE 12 NOVEMBA, 2026

**Arusha, 04 Novemba, 2026**

Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA) inapenda kuwajulisha Wadau wote kuwa kuanzia tarehe **12 Novemba, 2026** itaanza kutumia **mfumo wa Forodha wa TANCIS** (Tanzania Customs Integrated System) katika shughuli zake za forodha zinazohusiana na Afya ya Mimea na Viuatilifu.

## KUHUSU MFUMO WA TANCIS

TANCIS ni mfumo wa kisasa wa forodha unaosimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Mfumo huu utarahisisha, kuharakisha wa huduma na kuongeza ufanisi wa usimamizi wa shehena zinazohusiana na udhibiti wa Afya ya Mimea na Viuatilifu.

## MABADILIKO MUHIMU

Kuanzia tarehe 12/11/2026, maombi yote ya huduma za forodha zinazohusiana na Afya ya Mimea na Viuatilifu ikiwemo usafirishaji nje na ndani ya nchi wa mimea, mazao, bidhaa za mimea, Viuatilifu na vifungashio vyake yatawasilishwa kupitia mfumo wa TANeSW.

Hivyo basi, Hati za kibali na ruhusa zinazotolewa na TPHPA zitasimamiwa na mfumo huu kwa njia ya kielektroniki.

**WADAU**

Wadau wahakikishe kuwa

(i) wamesajiliwa na kutumia mfumo wa TANeSW kulingana na taratibu za TRA na kupata mafunzo/msaada wa matumizi ya mfumo uliotolewa na Mamlaka husika, kabla ya tarehe rasmi ya kuanza kwa mfumo huu.

(ii) Wasafirishaji, Mawakala wa forodha, Wauzaji wa pembejeo za kilimo, Wasafirishaji wa mazao na Wananchi kwa ujumla, wahakikishe wanaandaa nyaraka zote muhimu kwa ajili ya kutumia mfumo wa TANeSW kwa wakati ili kuepuka usumbufu wowote katika shughuli za forodha.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana nasi 0800110031 au fika katika Ofisi za TPHPA zilizo karibu yako au tembelea tovuti yetu: www.tphpa.go.tz

***Tushirikiane kwa pamoja kwa ajili ya Afya ya Mimea, usalama wa chakula na maendeleo ya kilimo nchini.***

Imetolewa na

Oshingi Shilla Samballu
**KAIMU MKURUGENZI MKUU**